# KAMPENI YA SIKU 16 ZA UANAHARAKATI DHIDI UKATILI WA KIJINSIA, 2024

## Kuelekea Miaka +30 ya Beijing: CHAGUA Kutokomeza Ukatili wa Kijinsia.

## ASANTE KWA KUJUMUIKA NASI KATIKA KUADHIMISHA KAMPENI YA SIKU 16 ZA KUPINGA UKATILI WA KIJINSIA

Kuanzia tarehe 25 Novemba, Tanzania itaungana na wanaharakati kutoka kote ulimwenguni kuadhimisha Kampeni ya Siku 16 za Uanaharakati Dhidi ya Ukatili wa Kijinsia. Kampeni hii huazimishwa kila mwaka kuanzia tarehe 25 Novemba ambayo ni Siku ya Kimataifa ya Kupinga Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto na kumalizika tarehe 10 Desemba, Siku ya Kimataifa ya Haki za Binadamu. Kipindi hiki cha Siku 16 ni fursa muhimu ya kutafakari kuhusu madhara ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto na kuchukua hatua madhubuti ili kukomesha vitendo hivyo.

### CHIMBUKO LA KAMPENI

Kampeni hii ilianza kutokana na harakati za wanaharakati wa kimataifa kupinga vitendo vyote vya ukatili wa kijinsia. Wanaharakati kutoka mabara mbalimbali, ikiwemo Ulaya, Amerika, Asia, na Afrika, walishirikiana kwa nguvu na kushinikiza utambuzi wa haki na ulinzi wa wanawake ili kupunguza ukatili waliokuwa wakifanyiwa. Mfano maarufu wa ukatili huu ni mauaji ya wanawake wa Mirabal yaliyofanyika mwaka 1960 nchini Dominica.

Mnamo Novemba 25, 1991, Umoja wa Mataifa ulitangaza rasmi siku hiyo kuwa Siku ya Kimataifa ya Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake. Kampeni ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia huanza siku hiyo na kuhitimishwa Desemba 10, ambayo ni Siku ya Kimataifa ya Haki za Binadamu. Lengo la kuanzia na kumaliza kampeni hii kwa siku hizi muhimu ni kuonyesha kuwa ukatili dhidi ya wanawake ni ukiukwaji wa haki za binadamu na kwamba unahitaji kushughulikiwa kama suala la haki za msingi za kila mtu.

Mwaka huu unasherehekea kumbukumbu ya Miaka 25 tangu Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa litamke Novemba 25 kuwa Siku ya Kimataifa ya Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake, ikiwa ni kumbukumbu ya dada wa Mirabal, ambao walifariki kikatili kwa kupigwa risasi siku hii mwaka 1960. Mnamo mwaka 2024, wanawake na wasichana bado wanaendelea kuuawa kwa sababu ya jinsia yao. Wanawake walioko kwenye nafasi za umma, ikiwa ni pamoja na wanasiasa, watetezi wa haki za binadamu, na waandishi wa habari, mara nyingi wanakuwa malengo ya vitendo vya makusudi vya vurugu, ama mtandaoni au mtaani, na baadhi ya vitendo hivi husababisha madhara makubwa na vifo vya makusudi.

Kampeni ya Siku 16 pia hujumuisha siku nyingine za kimataifa ambazo zina umuhimu mkubwa katika kulinda haki za wanawake. Miongoni mwa siku hizi ni:

- **Novemba 29,** Siku ya Kimataifa ya Watetezi wa Haki za Binadamu Wanawake.
- **Desemba 1**, Siku ya UKIMWI Duniani.
- **Desemba 3,** Siku ya Watu Wenye Ulemavu.
- **Desemba 6,** Siku ya Kukumbuka Mauaji ya Kikatili ya Montreal 1989 ambapo wanawake 14 waliokuwa wakisomea uhandisi waliuawa kwa chuki dhidi ya wanawake.
- **Desemba 10**, Siku ya Haki za Binadamu.

Hivyo basi, kipindi hiki cha Siku 16 kinatoa fursa ya pekee kwa jamii nzima, ikiwemo serikali, mashirika ya kijamii, na watu binafsi, kutambua na kukemea ukatili dhidi ya wanawake kama ukiukwaji wa haki za binadamu na kuchukua hatua ya kuutokomeza.

Siku hizi 16 za Uanaharakati dhidi ya Ukatili wa Kijinsia zimekuwa chombo muhimu kinachotumiwa na wadau duniani kote kutoa wito wa kutokomeza aina zote za ukatili dhidi ya wanawake na watoto kwa njia zifuatazo:

1. **Kuelimisha Umma**; kukuza uelewa wa jamii kuhusu ukatili wa kijinsia kama uvunjaji wa haki za binadamu, wenye athari katika ngazi za kijamii, kitaifa, kikanda na kimataifa.
2. **Kuimarisha Jitihada za Ngazi ya Msingi**; kukuza juhudi za kutokomeza ukatili wa kijinsia katika ngazi za chini na kuunganisha mipango na shughuli zinazoendeshwa katika maeneo mbalimbali ili kusaidia kuwawezesha wanawake kiuchumi.
3. **Kubadilishana Taarifa na Uzoefu;** kutoa fursa ya kushirikishana taarifa na uzoefu kati ya wadau mbalimbali kuhusu mbinu na changamoto katika mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia.
4. **Kuonyesha Mshikamano wa Dunia Nzima;** kuleta mshikamano na kuonyesha umoja katika juhudi za kutokomeza ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake, kwa lengo la kuleta mabadiliko chanya.
5. **Kupaza Sauti ya Kiharakati;** kutumika kama jukwaa la kupaza sauti ili kuhakikisha wadau wote wanatekeleza majukumu yao katika vita dhidi ya ukatili wa kijinsia.
6. **Kuwawajibisha Wenye Mamlaka;** kushinikiza mamlaka husika kutekeleza ahadi zao na kuweka mikakati ya kudumu ya kuzuia na kutokomeza ukatili wa kijinsia kwa vitendo.

Siku hizi **16 za uanaharakati** zinatoa nafasi ya kipekee kwa jamii kuungana kwa pamoja na kuchukua hatua zinazolenga kumaliza ukatili wa kijinsia na kujenga dunia yenye usawa na haki kwa wote.

## HALI YA UKATILI WA KIJINSIA NCHINI TANZANIA

Kwa mujibu wa ripoti ya Utafiti wa Hali ya Idadi ya Watu na Afya, 2022 (Tanzania Demographic Health Survey, 2022) inaonyesha kwamba asilimia 27% ya wanawake wenye umri kati ya miaka 15-49 wamekumbwa na vitendo vya ukatili wa kimwili kuanzia walipokuwa na miaka 15, huku asilimia 12% wakiwa wamewahi kukumbana na vitendo vya ukatili wa kingono. Kwa upande wa ukatili wa majumbani, asilimia 39% ya wanawake wameripoti kukumbana na vitendo vya ukatili kutoka kwa wenza wao wa sasa ama waliopita. Aidha, ripoti hii inaonyesha asilimia 8% ya wanawake wenye umri kati ya miaka 15-49 wamekeketwa. Kwa upande mwengine, wanawake zaidi wameripoti kufanyiwa vitendo vya ukeketaji wakiwa chini ya umri wa mwaka 1 ni asilimia (34%) huku waliokuwa na umri wa miaka 15 na zaidi ni asilimia (20%).

Kama inavyopendekezwa na ushahidi wa kimataifa na kuthibitishwa na ripoti ya TDHS 2022, wahusika wa kawaida wa ukatili wa kimwili au wa kijinsia mara nyingi ni wenzi wa ndoa au washirika wa karibu.

Wanawake wawili kati ya watano waliowahi kuwa na wenzi wamepitia ukatili uliofanywa na mume au mshirika wa karibu wa sasa au wa hivi karibuni, ukiwemo ukatili wa kimwili, kijinsia, au kihisia.

Katika miezi 12 iliyopita, asilimia 33% ya wanawake waliowahi kuwa na wenzi walipata ukatili kutoka kwa mume au mshirika wa karibu. Hii inajumuisha asilimia 22% waliopata ukatili wa kihisia, asilimia 24% ukatili wa kimwili, na asilimia 9% walipata ukatili wa kijinsia.

Uwepo wa vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa kiasi kikubwa unachangiwa na mfumo dume na kukosekana kwa ulinganifu wa mgawanyo wa majukumu ya kijamii baina ya wanawake na wanaume. Hali hii pia husababisha wanawake kushindwa kushiriki katika fursa mbalimbali kama vile za kiuchumi na uongozi na kuchochea zaidi ukandamizwaji. Umasikini pia, hutajwa kuchochea vitendo vya ukatili wa kijinsia mathalani vitendo vya ukeketaji na ndoa za utotoni.

## KAULI MBIU

Kauli mbiu ya Kampeni ya mwaka 2024 ni ***"Kuelekea Miaka 30 ya Beijing; CHAGUA kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Wasichana."*** Kauli mbiu hii inatoa wito wa dhati kwa kila mmoja wetu kuchukua hatua thabiti katika familia, jamii, au taasisi yetu ili kuzuia vitendo vya ukatili wa kijinsia. Inasisitiza umuhimu wa kila mtu kutumia nafasi yake katika kuleta mabadiliko kwa kuhakikisha wanawake na wasichana wanapata ulinzi wa kutosha dhidi ya ukatili wa kijinsia. Aidha, kauli mbiu hii inasisitiza kwamba vitendo vya ukatili vinapozuiwa mapema, tunafanikiwa kujenga jamii salama na yenye usawa, kwani kinga ni bora kuliko tiba. Hivyo, kila mmoja anahimizwa kuchagua kuchangia katika kumaliza ukatili dhidi ya wanawake na wasichana kwa vitendo thabiti.

Wakati tunapokaribia mwaka 2030, ambapo dunia imejizatiti kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), ikiwemo kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana (VAWG), na mwaka wa 30 wa Azimio la Beijing, Kampeni ya mwaka huu itatekelezwa chini ya kauli mbiu inayosema, "Kuelekea Miaka 30 ya Azimio la Beijing na Jukwaa la Hatua: Ungana ili Kuelekea Kumaliza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana." Kampeni hii inawahimiza wadau wote, hususan Serikali na sekta binafsi, kuchukua hatua kuhusiana na vipaumbele vya kupambana na Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana, kama ilivyopitishwa katika mapitio ya miaka 30 ya utekelezaji wa Jukwaa la Beijing na Azimio la Kisiasa: kujitolea upya, uwajibikaji, na upatikanaji wa rasilimali. Hii ni pamoja na kutekeleza mikakati kamili kwa kushirikiana na mashirika yanayoshughulikia haki za wanawake, kutenga bajeti zinazohitajika, na kuripoti kwa ufanisi maendeleo ya kupambana na ukatili.

**Malengo ya Msingi ya Uhamasishaji ni:**

1. Kuwahimiza Nchi Wanachama kuharakisha utekelezaji wa mikataba ya kimataifa na ya kikanda, na kutekeleza sheria pamoja na mipango ya Kitaifa ya Hatua ya Serikali nzima ili kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana, kwa kutenga rasilimali zinazohitajika;
2. Kuitaka sekta binafsi kupitisha na kutekeleza sera za kupambana na Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana;
3. Kuwajibisha wahalifu kwa kuboresha utekelezaji wa sheria na sekta za haki, ikiwa ni pamoja na polisi wanaozingatia jinsia;
4. Kuhakikisha wanawake na makundi yaliyotengwa wanaweza kupata haki kwa njia inayozingatia jinsia, ambapo wanaweza kutafuta haki bila hofu ya athari mbaya;
5. Kuongeza uelewa kuwa Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana haukubaliki kamwe, kuunda jamii isiyovumilia ukatili kwa kubadilisha mitindo ya kijamii yenye madhara;

**SHIRIKI KATIKA KAMPENI HII:**

Namna unaweza kushiriki katika Kampeni ya Siku 16 za kupinga Ukatili wa Kijinsia.

- **Jiandikishe Kuhudhuria Uzinduzi.** Unaweza kujiandikisha kushiriki katika uzinduzi wa kampeni ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia utakaofanyika tarehe 25 Novemba 2024, Mkoani Dar es Salaam.
- **Shiriki katika mbio za kupinga Ukatili wa Kijinsia.** Jiunge na mbio maalum za kupinga ukatili wa kijinsia zitakazofanyika katika visiwa vya Zanzibar na sehemu mbalimbali za Tanzania Bara.
- **Pata banda la maonesho.** Unaweza kushiriki kampeni kwa kupata nafasi ya banda la maonesho katika viwanja hivyo siku ya uzinduzi ili upate fursa ya kuungana na jamii, kueleza shughuli zako, na kushiriki juhudi zako katika kukomesha ukatili wa kijinsia.
- **Shawishi familia, marafiki, majirani kushiriki katika kampeni.**
- **Shirikishana jumbe na picha** mbalimbali za kupinga Ukatili wa Kijinsia kupitia mitandao ya kijamii ili kampeni iweze kuwafikia watu wengi zaidi.
- **Onesha ishara ya Amani!** vaa fulana au shati lenye rangi ya chungwa (Orange).

**● Jiunge katika maadhimisho haya ya kampeni ya Siku 16 za kupinga ukatili wa Kijinsia popote pale unaposikia.**

- Anzisha mijadala katika maeneo ya jamii, vijiwe, sokoni, michezoni na vijiwe vya bodaboda dhidi ya mila potofu zinazobagua wanawake na wasichana katika kupata rasilimali na kushiriki katika nafasi za uongozi.
- Viongozi wa dini wanaweza kutumia nafasi zao kutoa mafundisho kwa waumini juu ya masuala ya ukatili wa kijinsia.
- Shawishi jamii yako juu ya fikra chanya kuhusu umuhimu wa ushiriki wa wanawake kushika nafasi za uongozi kisiasa katika ngazi ya kijiji, kata, tarafa na taifa kwa ujumla.
- Hamasisha wanawake na wasichana kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika ngazi za kijiji, kata, tarafa na taifa ili kuongeza juhudi ya kuleta maendeleo ya nchi na kufikia uchumi wa viwanda.

**Ungana nasi kwenye Mitandao ya Kijamii kupitia Akaunti zetu**

- *Badili rangi ya mpangilio wa tovuti na akaunti zako katika mitandao ya kijamii na kuwa rangi ya chungwa katika kipindi hiki cha siku 16 za kupinga Ukatili wa Kijinsia.*

**Ungana nasi kwenye mitandao ya kijamii kupitia akaunti zetu:**

- **FACEBOOK: www.facebook.com/16daysofactivismcampiagn_tz**
- **TWITTER (X): www.twitter.com/16daysofactivismcampiagn_tz**
- **INSTAGRAM: www.instagram.com/16daysofactivismcampiagn_tz**
- **WEBSITE: www.wildaftanzania.or.tz**

Jiunge na mazungumzo. Kuwa sehemu ya mabadiliko na uangalie maudhui yaliyoshirikishwa kupitia alama za reli (hashtags) zifuatazo:

- **#16DaysofActivism2024**
- **#TokomezaUkatili**

## WAPI PA KUPATA MSAADA?
## UNAPOFANYIWA VITENDO VYA UKATILI WA KIJINSIA AU KUONA MTU AKIFANYIWA VITENDO HIVYO BASI CHUKUA HATUA ZIFUATAZO:

1. Unapofanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia au kushuhudia tukio lolote la ukatili dhidi ya wanawake na wasichana, ni muhimu kuchukua hatua mara moja. Hapa chini ni maeneo rasmi ambapo unaweza kupata msaada:
2. Madawati ya Polisi ya Kijinsia; katika vituo vya polisi vya nchi nzima, kuna madawati maalum ya kijinsia (Police Gender Desks) ambapo waathirika wa ukatili wa kijinsia wanaweza kuripoti matukio yao kwa usiri na kwa msaada wa askari wa kike. Madawati haya yameanzishwa ili kuhakikisha kuwa taarifa za ukatili wa kijinsia zinachukuliwa kwa uzito unaostahili na kwa kuzingatia haki za waathirika.
3. Huduma za Mkono kwa Mkono (One Stop Centre); vituo vya huduma ya mkono kwa mkono vipo sehemu mbalimbali nchini, ambapo waathirika wa ukatili wanapata huduma za kisheria, matibabu, na ushauri wa kisaikolojia. Hizi ni huduma zilizojumuishwa katika sehemu moja kwa urahisi wa upatikanaji, ili mwathirika aweze kupata msaada wa haraka na kwa ufanisi.
4. Ofisi za Ustawi wa Jamii; ofisi hizi zipo katika halmashauri zote za wilaya na ni sehemu nyingine muhimu ya kuripoti vitendo vya ukatili. Watendaji wa ustawi wa jamii hutoa msaada wa kisheria, ushauri wa kijamii, na hudumia waathirika kwa kushirikiana na taasisi zingine zinazohusika.
5. Serikali za Mitaa na Vituo vya Afya; vituo vya afya vinatoa huduma muhimu kwa waathirika wa ukatili wa kijinsia, ikiwa ni pamoja na matibabu ya majeraha, ushauri wa kisaikolojia, na huduma zingine muhimu za afya. Aidha, viongozi wa serikali za mitaa wanahusika katika usimamizi wa masuala ya ukatili katika jamii na wanaweza kuwa msaada mkubwa kwa waathirika wanaohitaji kupeleka masuala yao mbele kwa njia rasmi.
6. Vituo vya Msaada wa Kisheria; nchi nzima imejaa vituo vya kutoa msaada wa kisheria kwa waathirika wa ukatili wa kijinsia. Vituo hivi vinatoa msaada wa kisheria bure kwa waathirika, ili kuwasaidia kufahamu haki zao na kuchukua hatua zinazostahili dhidi ya mkatili. Hii ni pamoja na kutoa msaada katika kutafuta fidia, kuhakikisha haki za waathirika zinaheshimiwa, na kuendelea na mchakato wa kisheria ili kuwawajibisha watuhumiwa.

Baadhi ya Asasi za Kiraia zinatoa msaada wa kisheria wa dharura. Piga bure namba zifuatazo:

- Women in Law and Development in Africa (WiLDAF), Piga Bure Namba: **0800780070.**
- Legal and Human Right Centre (LHRC), Piga Bure Namba: **0800750035**
- Tanzania Women Lawyers Association (TAWLA), Piga Bure Namba: **0700751010**
- Women and Legal Aid Centre (WLAC), Piga Bure Namba: **0800780100**

Lakini pia serikali ina namba maalumu kwa ajili ya kutoa taarifa maalumu kwa kupiga simu bure kama ifuatavyo
**113**-Namba maalum kwa ajili ya matukio ya rushwa ikiwemo rushwa ya ngono
**116**- Namba maalumu kwa ajili ya kuripoti matukio ya vitendo vya ukatili hasa kwa watoto.

Baadhi ya Applikesheni zinatoa msaada wa kisheria kupitia mtandao, pakua Applikesheni katika simu janja na uweze kupata msaada wa haraka kupitia Wanasheria na Wasaidizi mbalimbali wa kisheria

**Mifumo ya Mtandaoni:**

Pakua programu zifuatazo kwa msaada wa kisheria:

- *Funguka App*
- *Haki Kiganjani*
- *Sheria Kiganjani*
- *Haki Yangu*

**Tuchukue Hatua!**

Pamoja tunaweza kuzuia ukatili wa kijinsia. Ripoti matukio na linda haki za wahanga!

# SIKU 16 ZA UANAHARAKATI DHIDI UKATILI WA KIJINSIA

WiLDAF TANZANIA

Women in Law & Development in Africa

MKUKI UKATILI


MAWASILIANO:-

Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika (WiLDAF)

Mikocheni “A” , Mtaa wa WiLDAF,

Jengo F, Kitalu Na. 635, S.L.P 76215, Dar es Salaam - Tanzania

Simu Na: 255 022 2701995

Barua pepe: info@wildaftanzania.or.tz

Tovuti: www.wildaftanzania.or.tz | Mitandao ya kijamii: @willdaftz